# 216 NAFASI ingaliko arusini

## 216

1. Nafasi ingaliko arusini ita’yokuwa kwake Mungu Baba. Njoo kwake, nafasi ingaliko!

2.Njiani mwako jua linakuchwa, jioni inakaribia sasa. Njoo mbio, nafasi ingaliko!

3. Karamu ya arusi ni tayari, na Bwana anakualika wewe. Njoo mbio, nafasi ingaliko!

4. Wanaingia watu wengi huko, ufanye hima, uingie nawe! Njoo mbio, nafasi ingaliko!

5. Tazama, lango limefunguliwa, neema gani: Utakaribikshwa! Njoo mbio, nafasi ingaliko!

6.Ufike mbio, utaona heri, Yesu atoa wingi wa neema! Njoo mbio, nafasi ingaliko!

7.Je, utaona shangwe ya mbinguni? Bwana arusi akungoja sana. Njoo mbio, nafasi ingaliko!

8.Uliyesitasita unaitwa, ujiazimu kuja kwake Mungu! Njoo mbio, nafasi ingaliko!

9.Ukichelewa, lango litafungwa, na utalisisikia neno hili: “Ondokeni! Sikuwajua ninyi!”

H. Bonar